

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Simu Na: +255 026 216 0240
Nukushi: +255 (026) 2963629
Barua Pepe: ps@utumishi.go.tz

Tovuti: <http://www.utumishi.go.tz>

Unapojibu tafadhali taja:



Mji wa Serikali Mtumba
Mtaa wa Utumishi,
S.L.P. 670,
DODOMA.

Kumb. Na. CA. 178/311/02/1

24 Septemba, 2024

Makatibu Wakuu wote,
Makatibu Tawala wa Mikoa wote,
Wakuu wa Idara za Serikali Zinazojitegemea wote,
Watendaji Wakuu wa Wakala wa Serikali wote,
Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi za Umma wote,
Wakurugenzi wa Majiji, Manispaa na Miji wote,
Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya wote,
TANZANIA BARA.

Kuh: **KUWASILISHA TAARIFA ZA WATUMISHI WANAOHITAJI UHAMISHO
KWA LENGU LA KUWAFUATA WENZI WAO WA NDOA**

Tafadhali rejeeni kichwa cha habari kuhusu somo tajwa hapo juu.

2. Utaratibu wa uhamisho wa watumishi wa Umma kutoka kwa mwajiri mmoja kwenda kwa mwingine umefafanuliwa katika Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2008 kwenye Aya ya 4.17, Kifungu cha 8(3)(h) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 vikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 106(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, Kanuni D.56 ya Kanuni za Kudumu Katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009 na Aya ya 13(k) ya Taratibu za Uendeshaji Utumishi wa Umma za mwaka 2003.

3. Vifungu vya Sheria, Kanuni na Taratibu vilivyotajwa hapa juu, vinampa Katibu Mkuu (UTUMISHI) mamlaka ya kufanya uhamisho kwa watumishi miongoni mwa waajiri kwa nia ya kuwainisha rasilimaliwatu iliyopo na kila kunapokuwepo sababu zenye maslahi kwa Umma na ili kuboresha utendaji kazi Serikalini.

4. Mbali na sababu za uhamisho zenye maslahi kwa Umma, kupitia Waraka wa barua yangu wenye Kumb. Na. EA. 45/257/01/49 wa tarehe 31 Machi, 2006 Ofisi yangu ilitoa utaratibu kwa watumishi ambao wanazo sababu za

kuruhusiwa kuhama ikiwemo kuwafuata wenzi wao wa ndoa. Katika utekelezaji wa Waraka huu, watumishi wameendelea kuhama kwa lengo la kuwafuata wenzi wao wa ndoa. Hata hivyo, katika siku za hivi karibuni kumekuwepo na ongezeko kubwa kutoka kwa watumishi wanaoomba uhamisho kwa lengo la kuwafuata wenzi wao wa ndoa. Kutokana na hali hii na ili kuiwezesha Ofisi hii kuwa na taarifa kamili ya idadi ya watumishi wanaohitaji kuhama kwa lengo la kuwafuata wenzi wao wa ndoa mnaelekezwa kuwajulisha watumishi wenu kuwasilisha taarifa zao kwenu ili mziwasilishe taarifa hizo katika Ofisi hii kabla au ifikapo tarehe 05 Oktoba, 2024.

5. Taarifa hizo ziwasilishwe kwa nakala ngumu na laini kwa kuzingatia fomati iliyoambatishwa na barua hii. Aidha, nakala laini iwasilishwe kupitia barua pepe: thecla.gasembe@utumishi.go.tz. Kwa mawasiliano zaidi tafadhali wasiliana na Bi. Felister E. Shuli kwa namba ya simu: **0717414688**.

6. Ninawashukuru kwa ushirikiano wenu.



Juma S. Mkomi

KATIBU MKUU (UTUMISHI)

Nakala: Katibu Mkuu Kiongozi,
Ofisi ya Rais,
IKULU,
1 Barabara ya Julius Nyerere,
CHAMWINO,
S.L.P. 1102,
40400 DODOMA

[illegible]

- v Anocheti cha ndoa (Kiambatiawe kwenye mfumo wa e-Watumishi)
- x Hana cheti cha ndoa
- * Uthibitisho husika kiambatiawe kwenye mfumo wa e-Watumishi